

JINA.....NAMBA YAKO.....

JINA LA SHULE.....SAHIHI.....

102/3

KISWAHILI

KARATASI LA 3

FASIHI

JULAI/AGOSTI

MUDA: SAA 2 ½

## **MTIHANI WA MWIGO KAUNTI NDOGO YA KAKAMEGA KUSINI-2016**

*Hati ya Kuhitimu Masomo ya Sekondari – Kenya (K.C.S.E)*

102/3

KISWAHILI

KARATASI LA 3

FASIHI

### **MAAGIZO**

- a) Jibu maswali manne pekee.
- b) Swali la kwanza ni la lazima.
- c) Usijibu zaidi ya swali moja kutoka sehemu moja.
- d) Mtihani huu una jumla ya alama 80.

*Hii karatasi ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.*

*Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote nne za karatasi hii ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

## **SEHEMU YA A**

### **SWALI LA LAZIMA: FASIHI SIMULIZI**

1. i) Tofautisha vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi (al.4)
  - a) Ngoma na ngomezi
  - b) Mighani na ngano za mashujaa
- ii) Taja aina nne za ngomezi kwa kipindi cha sasa. (al.2)
- iii) Fafanua sifa nne za mlumbi. (al.4)
- iv) Linganua vitendawili na methali (al.8)
- v) Andika sifa mbili za maapizo. (al.2)

## **SEHEMU YA B**

### **KIDAGAA KIMEMWOZEA**

2. Riwaya ya kidagaa imeangazia maudhui ya utengano. Thibitisha. (al.20)

## **AU**

3. “Mimi si mwerevu sana lakini pia si mjinga wa mwisho.”
  - a) Eleza muktadha wa dondo hili (al.4)
  - b) Eleza sifa za msemaji (al.6)
  - c) Mzungumziwa anaendeleza maudhui ya usiri. Thibitisha. (al.10)

## **SEHEMU YA C: MSTAHIKI MEYA**

4. “Haina haja kuniondoa. Ugeniambia kuondoka ningeondoka tu.”
  - a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (al.4)
  - b) Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (al.8)
  - c) Toa ithibati kuwa nchi ya cheneo imejaa ufisadi. (al.8)

## **Au**

5. Jadili jinsi maudhui ya usaliti yanavyofafanuliwa katika tamthilia ya mstahiki Meya. (al.20)

## **6. SEHEMU YA D: USHAIRI**

(al.20)

SIGOMBE KIVULIE

Ndege akiwa angani ,usiseme wangu mie  
Mngoje atue chini, na ndipo mgombanie  
Lakini yupo hewani,tama isikwingie  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

Ndege apaa angani,sigombee kivulie  
Manapigana machoni, mwagombea uzurie  
Mwalizana kama nyani,matunda mwagombee  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

Shika awe mkononi,ndipo ukajivunie  
Umshikapo mwilini,chukua kajifugie  
Kama utavyo moyoni,kufuga kajifugie  
Kama utavyo moyoni,kufuga ama mwachie  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

Usimlilie nyuni,kwanza akukaribie  
Na sauti mdomoni,aimbapo usifie  
Saburi ndicho kiini,kila jambo sivamie  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

Mwaingia ushindani,kwa magumu mpanie  
Ninyi nyote ufukani,ndege juu muanie  
Ndege atatualini?, pengine ajiendee  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

Siingie ujingani,majambo mfikirie  
Sirukie kifanani,ndege juu muanie  
Utafanywa hayawani,jirani wakubeue  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

Atuapo matawini,kwa jicho kuangalie  
Awaone dharauni,na mbawa awapigie  
Na mate yamo kinywani,katu asiwasogee  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

Kaditama upigani,akheri amuambae  
Wawindaji pendaneni,mwachie ndege apae  
Lisha aliye tunduni,wa juu sitegemee  
Sigombee kivulie,ndege apaa angani.

***Maswali***

- (a) Eleza dhamira ya shairi hili (al.2)
- (b) Taja na utoe mifano ya mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili (al.4)
- (c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari (al.4)
- (d) Eleza jinsi uhuru wa mtunzi unavyojitokeza katika shairi. Tolea mifano jibu lako (al.4)
- (e) Eleza umbo/muundo wa shairi hili (al.4)
- (f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi (al.2)
  - (i) Nyuni
  - (ii) Wakabue

**SEHEMU YA E: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

7. Msiba unaowapata wanawake katika diwani hii ni wa kujitakia. Thibitisha kwa kurejelea wahusika wafuatao;

- a) Jamila (al.4)
- b) Sela (al.4)
- c) Christine (al.4)
- d) Lucy (al.4)
- e) Kudura (al.4)